NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

3 Januari 2022

Kwa Washauri Wasaidizi wote kote ulimwenguni

Marafiki Wapendwa sana,

Kwenye siku hii ambapo tulisubiri kwa matazamio makubwa sana kuwakaribisheni ninyi nyote katika Nchi Takatifu kwa ajili ya kongamano la pamoja na wajumbe wa Bodi za Washauri wa Bara, tunajisikia kusukumwa kuwaandikieni na kuelezea huzuni yetu kwamba, kwa sababu ya hali za ulimwengu, mkusanyiko huu uliongojewa kwa shauku kubwa hauwezi kufanyika. Mawazo tuliyotarajia kuwaelezea ana kwa ana sasa lazima yawasilishwe kutokea mbali. Lakini umbali haupunguzi nguvu ya upendo tulionao kwa kila mmoja wenu.

Leo ni miaka mia moja tangu kusomwa kwa mara ya kwanza hadharani kwa Wasia na Agano la ‘Abdu’l-Bahá. Katika Waraka huo wa thamani kubwa, Yeye aliweka wajibu wa Mikono wa Hoja ya Mungu, ambapo kwa msaada wake Bodi za Washauri Wasaidizi wa Uenezi na Ulinzi kwa mara ya kwanza zilianzishwa. ‘Abdu’l-Bahá aliwataka Mikono wa Hoja “kueneza Manukato Matakatifu, kuadilisha roho za watu, kukuza ujifunzaji, kuboresha tabia za watu wote na katika nyakati na hali zote, kuwa waliotakasika na waliojitenga kutokana na mambo ya kidunia.” Kuyasoma maneno haya kwa wakati huu huamsha kwa ajili yetu huduma ambayo kila mmoja wenu anaifanya katika ulimwengu mzima wa Kibahá’í. Hakika, jumuiya ya Kibahá’í ya ulimwengu inawiwa shukrani kwa asasi yote ya Washauri, wakiwemo wale wote ambao wamehudumu kama Washauri wa Bara, Washauri Wasaidizi na wasaidizi kwa miaka iliyopita. Bila huduma kama hii ya kujitoa kutoka kwa wengi mno, maendeleo ya kushangaza yaliyofanywa katika miongo ya hivi karibuni, ambayo leo yapo dhahiri ulimwenguni, yasingekuwa yametokea. Na mchango wa lazima kwa ajili ya maendeleo hayo umekuwa ndiyo muongozo na hamasa iliyotolewa na Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa: asasi nyumbufu na nyepesi kuelewa na kukata shauri, na isiyochoka kabisa.

Hadi sasa mmekuwa na fursa ya kujifahamisha maelekezo ya Mpango wa Miaka Tisa na kutafakari kwa kina juu ya matokeo yake. Kama itakavyokuwa dhahiri, mlolongo wa nyanja ambazo waumini wanaombwa kuhudumu ndani ya klasta zao, ili kuachilia nguvu ijengayo jumuiya ya Imani katika viwango vikubwa zaidi, umepanuka. Kwa kulinganishwa, mlolongo wa mambo ambayo kwayo lazima muyape umakini mkubwa nayo umepanuka. Jitihada zenu ni za lazima kwa ajili ya kazi ya kukuza uwezo wa kuchangia kwenye maeneo mbalimbali ya jitihada ya jumuiya ya Kibahá’í, na jitihada zenu ni za lazima katika kuwasaidia marafiki kudhihirisha kwa vitendo uwezo walioupata. Katika kuyashughulikia mahitaji haya mawili, na kwa jumla zaidi katika kutimiza majukumu yenu ya elimu na uboreshaji wa tabia, ninyi bila shaka kwa kiasi kikubwa mnategemea ufanisi wa mchakato wa taasisi. Tangu kuanzishwa kwake,

taasisi imekuwa chombo muhimu kwa ajili ya kazi yenu, na vivyo hivyo, msaada wenu wa nguvu umekuwa muhimu kwa maendeleo yake. Inatupa furaha, hivyo, kuona moyo wa ushirikiano thabiti, wenye ari ambao hupambanua uhusiano wenu na wale wote wanaohusika na kuratibu jitihada za taasisi.

Hakuna shaka mmesoma maelekezo tuliyowasilisha katika ujumbe wetu kwa Washauri siku chache zilizopita, wa jinsi ambavyo lazima muwasaidie marafiki kupata muitikio unaofaa kwa kila mojawapo ya changamoto nyingi wanazokabiliana nazo katika utekelezaji wao wa Mpango. Kuhuaiana na hili, tunajisikia kuwa na yakini kwamba mnatambua kuwa, hata ushauri wenu uwe na manufaa jinsi gani, athari ya mfano wenu bado itakuwa kubwa zaidi. Nguvu itambulikayo ya ofisi yenu ni kwamba inawaunganisha marafiki na viwango tofauti tofauti vya utawala wa Kibahá'í na kukuza moyo wa ushirikiano ambao huwaweka pamoja. Mnalo jukumu muhimu kusaidia kukuza ufahamu wa kusudi la utawala wa Kibahá'í na kusaidia uanzishwaji na utendaji ufaao wa Mabaraza mapya ya Kiroho ya Mahali. Mnaendelea kuwaunganisha marafiki na mipango na miradi ya asasi za Kibahá'í zitendazo kazi kwenye ngazi za mahali, kanda na kitaifa. Hatimaye, mnaimarisha uhusiano baina ya marafiki na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa kuhamasisha na kuongoza ujifunzaji wa jumbe kadiri zinavyokuja. Waumini wanawaangalieni ninyi kwa ajili ya kupata uelewa mzuri wa Mpango na kwa ajili ya mfano wa kijasiri wa jinsi ya kuweka maelekezo yake katika utendaji, hususan katika kufundisha Imani. Ufahamu wenu thabiti wa uhalisia wa hali zilivyo katika klasta mbalimbali, ukichanganywa na uelewa wenu kikamilifu wa kile kihitajikacho ili Hoja isonge mbele, huwaweka katika nafasi nzuri ya kutoa michango ya kiuangalifu, kibunifu na ya wakati kwa ajili ya ushauriano kuhusu namna ya kuachilia nguvu ya Imani ijengayo jamii katika kila mazingira.

Kwa kuongezea yaliyoelezwa hapo juu, tunapenda kuwaelekeza wajibu wenu maalum katika kuwahamasisha vijana. Vijana wengi ambao sasa wanapata ushindi kwa ajili ya Hoja walivutiwa na Washauri Wasaidizi au wasaidizi ambao shauku yao ya kusaidia na moyo wa kujitoa viliwafundisha kutegemea juu ya nguvu ya mathibitisho matakatifu na kwa ushujaa kuingia katika uwanja wa huduma. Wajibu wenu unaenda hata mbali zaidi hadi kwenye uendelezaji wa elimu ya watoto na vijana chipukizi, kwenye uinuaji wa vijana wadogo, na kwenye uimarishaji wa mtindo wa maisha ya familia ambao kizazi hadi kizazi utatoa roho zilizojiweka wakfu, wafuasi waaminifu wa Bahá'u'lláh ambao wamechagua uboreshaji wa ulimwengu dhidi ya uendekezaji wa raghba binafsi. Vijana ambao, katika mwaka wa mwisho wa Mpango wa Miaka Tisa, watakuwa wanatekeleza vitendo vya huduma ili kuhakikisha mafanikio yake ya mwisho kwa namna nyingi ni watoto ambao, leo, wanahitaji kulelewa katika upendo wao wa Uzuri Uliobarikiwa na uelewa wao wa utume Wake.

Marafiki wapendwa, katika nyakati zenu za sala, muwe na hakika kwamba maombi yenu yote kwa Bahá'u'lláh yanaandamana na maombi yetu wenyewe katika Makaburi Matakatifu kwa niaba yenu. Mjongeo wenu na utuli wenu na viongozwe na pepo nyororo za Mapenzi Yake, na aweze kujalia juu yenu baraka zidumuzo za kuwezeshwa kumtumikia Yeye kulingana na matakwa Yake.

**IMESAINIWA NA NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU**